



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**  
**IDARA YA WANYAMAPORI**



**CHUO CHA MAFUNZO YA UHIFADHI WA MALIASILI KWA JAMII -  
LIKUYU SEKAMAGANGA**

**TANGAZO LA KOZI KWA MWAKA 2021/2022**  
**ASTASHAHADA YA AWALI YA WAONGOZA WATALII**

Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga ni miongoni mwa vyuo vilivyoko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Chuo kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya ufundi nchini (NACTE) kwa **usajili namba REG/SAT/46**.

Mkuu wa Chuo anapenda kuutangazia umma wa watazania na waombaji wenye sifa kutuma maombi ya kujiunga na mafunzo ya kozi ifuatayo;

1. **JINA LA KOZI:** Astashahada ya awali ya Waongoza watalii – NTA 4.
2. **MUDA WA MAFUNZO:** Mwaka mmoja (1).
3. **SIFA ZA KUJIUNGA:**
  - i) Mhitimu wa kidato cha nne mwenye cheti chenye ufaulu usiopungua alama D kwa masomo manne ikiwemo Baiolojia na Kiingereza au Jiografia **AU**
  - ii) Mhitimu mwenye cheti cha VETA (VTA III) katika fani ya Utalii na wanyamapori kutoka katika Chuo chochote kilichosajiliwa na VETA.

**4. TARATIBU ZA UOMBAJI:**

i) Waombaji wanatakiwa kujaza fomu ya maombi na kuiwasilisha kwa Mkuu wa Chuo baada ya kuambatanisha nakala za vyeti vyote vinavyotakiwa. Fomu za maombi zinapatikana katika tovuti ya chuo ya [www.cbctklikuyu.ac.tz](http://www.cbctklikuyu.ac.tz) . Pia katika Ofisi za Wizara ya Maliasili na Utalii za Dodoma zilizoko eneo la mtumba (Mji wa Kiserikali) na Swagaswaga, Ofisi ya Utalii Kanda kusini (Iringa), Ofisi ya Afisa wanyamapori Mkoa wa Ruvuma, Ofisi za Maafisa wanyamapori wa Wilaya za (Namtumbo, Songea, Mbinga, Nyasa, Tunduru), Jumuiya ya Hifadhi za (Mbarang'andu, Kimbanda , Kisungule, Nalika na chingoli).

ii) Waombaji watachaguliwa kulingana na kigezo cha ufaulu wao.

**5. ADA YA MAFUNZO:** Shilingi Milioni mbili laki moja na elfu sita tu (**Tsh. 2,106,000/=**) ambayo inagharamia mafunzo ya nadharia na vitendo, malazi na chakula. Ada inaweza kulipwa kwa awamu mbili.

**6. TAFADHALI ZINGATIA YAFUATAYO:**

- i) Malipo yote yafanyike kupitia account ya Chuo iliyopo **benki ya NMB**, Jina la akaunti **CHUO CHA LIKUYU SEKAMAGANGA, NAMBA YA AKAUNTI 62401100011**.
- ii) Ada ya maombi ni shilingi elfu kumi (10,000/=) na italipwa na muombaji kupitia akaunti ya chuo. Baada ya kulipa, muombaji ataambatanisha risiti ya benki inayoonesha malipo hayo pamoja na fomu ya maombi ya kozi wakati wa kurudisha. Ada hii hairudishwi (non-refundable).
- iii) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30 Septemba 2021.

**Kwa ufafanuzi zaidi wasiliana na;**

**Mkuu wa Chuo,**

CBCTC-Likuyu Sekamaganga,

S.L.P 24,

Namtumbo, Ruvuma.

Simu ya mezani: 025 295 1050,

Simu za mkononi: 0754 352 846/0788 409 433, Barua pepe: [cbctc@maliasili.go.tz](mailto:cbctc@maliasili.go.tz)